Wimbo:

Nitainua macho yangu, nitazame milima
Msaada wangu utatoka waapi;
Msaada wangu u katika Bwana.

Bwana Ameumba mbingu na Nchi
Asiiuache mguu wako usongezwe
Haasinzii yeye akulindaye
Haoni usingizi

Bwana atakulinda na mabaya yote
Yeye atailinda nafsi yako
Utokapo na ungiapo wewe
Bwana atakulinda.

Bwana ndiye mlinzi wako daima
Yeye uvuli mkono wako wakuume
Utokapo na uingiapo wewe
Bwana atakulinda.

Sala ya Bwana:

Watu wote: Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe,
Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe,
hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu.
Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe
waliotukosa. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.
Amin.

Sala

***Mhudumu*:** Mwenyezi Mungu, ambaye kwako wewe mioyo yote
I wazi, haja zote zimejulikana, wala hakuna la siri lililositirika:
Uyasafishe mawazo ya mioyo yetu kwa kutuvuvia roho wako
Mtakatifu, ili tukupende kwa ukamilifu. Na kulitukuza Jina lako
takatifu kama itupasavyo; Kwa Kristo Bwana wetu. Amin.

Mhudumu. Mungu alinena maneno haya akasema: Mimi ni
Bwana, mungu wako; usiwe na miungu mingine ila mimi.

Watu*:* Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa
kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani,
wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala
kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana Mungu wako, ni Mungu
mwenye wivu, nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi
cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu
elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

Watu.: Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu.: Usilitaje bure Jina la Bwana , Mungu wako: maana
Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia, mtu alitajaye jina lake
bure.

Watu: Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu: Ikumbuke siku ya sabatu uitakaze. Siku sita fanya
kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya
Bwana, Mungu wako; siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe,
wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala
mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye
ndani ya mlango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya
mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku
ya saba ; kwa hiyo Bwana akaibariki siku ya sabato, akaitakasa.

Watu: Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu: Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako
zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu
wako.

Watu. Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu: Usiue

Watu: Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu: Usizini.

Watu: Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu: Usiibe

***Watu*:** Bwana, uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu. Usimshuhudie jirani yako uongo.

Watu: Bwana uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Mhudumu: Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke
wa jirani yako, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala
ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho
jirani yako.

Watu: Bwana uturehemu, utuelekezee mioyo, tuishike amri hii.

Sala ya Siku

Wimbo

Watu wote: NAMWAMINI Mungu mmoja, Baba mwenyezi,
Muumba wa mbingu na nchi na vitu vyote vinavyoonekana na
visivyoonekana: Na Bwana mmoja Yesu Kristo, Mwana pekee
wa Mungu, Mwana wa azali wa Baba, yu Mungu kutoka katika
Mungu, yu Nuru kutoka katika Nuru, yu Mungu kweli kutoka
katika Mungu kweli, yu Mwana wa azali, hakuumbwa, mwenye
uungu umoja na baba, kwa yeye huyu vitu vyote viliumbwa:
aliyeshuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu wanadamu, na kwa
wokovu wetu, akafanyika mwili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu
katika Bikira Mariamu, akawa mwanadamu. Akasulibiwa kwa
ajili yetu, zamani za Pontio Pilato. Aliteswa, akazikwa, siku ya
tatu akafufuka kama yanenavyo Maandiko Matakatifu, akapaa
mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa Baba. Naye atakuja tena
kwa utukufu kuwahukumu watu walio hai nao waliokufa: na
miliki yake haina mwisho.
Namwamini Roho Mtakatifu, Bwana, Mtoa uzima, atokaye
katika Baba na Mwana, anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na
Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii. Naamini
Kanisa moja takatifu, Katholiko* Apostoliko+. Nakiri ubatizo
umoja wa kuondolea dhambi. Natazamia kufufuliwa kwa wafu,
na uzima wa zamani zijazo. Amin.

**Kanisa Katholiko, maana yake ndiyo ushirika wa wote wamwaminio Bwana, wa nyakati zote na mahali pote.*
+Kanisa Apostoliko, maana yake ndiyo kanisa lililonjengwa juu ya msingi wa mafunzo ya mitume.
(Tazama Waefeso 2:20)

Hotuba

Mhudumu: Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa
ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama
alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa
lazima; Maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa
ukunjufu.

Wimbo wa Sadaka

***Mhudumui** : Tuliombee Kanisa la Kristo lote pia lililo vitani hapa duniani*.

Mhudumu: Mwenyezi Mungu uishiye milele, uliyetufundisha
kwa mtume wako mtakatifu tuombe na kutoa shukrani kwa ajili
ya watu wote: Twakusihi kwa unyenyekevu kwa rehema yako
kuu upokee *sadaka na matoleo yetu* na kuyasikia maombi yetu
haya, tunayotoa kwako Mwenyezi Mungu;

Watu: Twakusihi, utusikie, Bwana mwema

Mhudumu: Twakuomba sana, ulivuvie daima Kanisa la ulimwenguni mote roho ya kweli, na ya umoja na ya mapatano: Uwajalie wote wanaokiri Jina lako takatifu, wapatane katika kweli ya Neno lako takatifu na kuishi kwa umoja na upendano. Tena twakusihi uwaokoe na kuwalinda watawala wetu ili tutawaliwe nao kwa kicho na utulivu. Uwajalie wote walio na mamlaka na madaraka chini yao, wakate mashauri na kutoa hukumu kwa haki pasipo upendeleo, kwa kuwaadhibu wahalifu na waovu,na kuimalisha dini yako ya kweli, na mambo yote yalio mema.

Watu: Twakusihi, utusikie, Bwanamwema

Mhudumu: Baba wa mbinguni, uwape neema maaskofu na wote wachungao roho za watu, ili kwa mwenendo wao na mafundisho yao walitangaze Neno lako la kweli lililo hai, na kuzihudumia Sakramenti zako takatifu; kwa haki na jinsi ilivyo kanuni. Na watu wako wote uwakirimie neema yako ya mbinguni; na hasa kwa waliopo hapa, ili, kwa mioyo ya unyenyekevu na ibada, walisikie na kulipokea Neno lako takatifu; wakutumikie kwa kweli katika utakatifu na haki siku zote za maisha yao.

Watu: Twakusihi, utusikie, Bwanamwema

Mhudumu: Nasi kwa unyenyekevu twakusihi, kwa wema wako, Bwana, uwafariji na kuwasaidia wote waliopatwa na taabu, huzuni, umaskini, ugonjwa au shida nyingine yo yote ya maisha haya yasiyodumu. Twalitukuza Jina lako takatifu, kwa ajili ya watumishi wako wote, waliofariki dunia katika imani yako na kicho chako; tukikusihi utupe neema, tufuate vielelezo vyao vyema, tushiriki pamoja nao ufalme wako wa mbunguni: utujalie hayo Baba, kwa ajili ya Yesu Kristo, ambaye pekee ni mpatanishi na Mwombezi wetu. Amin.

Mhudumu: Wapendwa katika Bwana, mlio na nia kuujia Ushirika Utakatifu wa mwili na damu ya Mwokozi wetu Kristo, imewapasa kutafakari jinsi Paulo Mt. awaonyavyo watu wote wajipime kwa bidii, na kujichunguza, kabla hawajathubutu kuula Mkate huu na kukinywea Kikombe hiki. Basi , ndugu zangu, jihukumuni nafsi zenu, msije mkahukumiwa na Bwana; tubieni dhambi zenu; mwaminini Kristo Mwokozi, kwa imani iliyo hai na thabiti;tengenezeni mienendo yenu, mwe na upendano ulio kamili na watu wote. Na zaidi ya yote, hamna budi kumshukuru Mungu, Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, kwa unyenyekevu, kwa vile aliyoukomboa ulimwengu kwa mauti na mateso ya Mwokozi wetu Kristo, Mungu tena Mwanadamu. Hayo alitenda atufanye kuwa wana wa Mungu, atukweze kwenye uzima wa milele. Anataka sisi tukumbuke daima pendo hili bora sana la Mwalimu na Mwokozi wetu pekee Yesu Kristo alietufilia hivi. Basi, ameagiza siri hizi takatifu ziwe arabuni ya pendo lake, na ukumbusho wa daima wa kufa kwake, kwa faraja yetu kuu isiyo na ukomo. Kwake basi, na kwa Baba, na kwa Roho Mtakatifu tutoe shukrani ya daima, kama ilivyo wajibu; tukitii kwa moyo wote mapenzi yake matakatifu na kufanya bidii kumtumikia katika utakatifu na haki ya kweli siku zote za maisha yetu. Amin.

Kwa wote waliokuja kuupokea Ushirika Utakatifu,

Kasisi*:* Ninyi nyote mlio na toba ya kweli na la moyo, mlio na upendano na majirani zenu, mnaokusudia kuishi maisha mapya, na kuzitii amri za Mungu, na kuenenda tangu leo katika njia zake takatifu; karibuni kwa imani, pokeeni Sakramenti hii takatifu kwa faraja yenu;ungameni mbele ya Mwenyezi Mungu, mkipiga magoti kwa unyenyekevu.

Watu Wote: MWENYEZI Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Muumba vitu vyote, Mhukumu watu wote; twaungama na kuzililia dhambi zetu na maovu yetu ya kila namna, tuliyoyatenda kwa ubaya mno mara kwa mara, kwa mawazo na maneno na matendo tumekuchukiza wewe, Mwenyezi Mungu, na kujivutia kwa haki ghadhabu yako. Twatubu kweli, na kuyasikitikia sana haya makosa yetu; tukiyakumbuka tuna huzuni; mzigo wake hauchukuliki. Uturehemu, uturehemu, Baba mwenye rehema nyingi; kwa ajili ya Mwana wako, Bwana wetu Yesu Kristo, utusamehe yote yaliyopita; utuwezeshe tangu leo kukutumikia na kukupendeza katika upya wa maisha, kwa heshima na utukufu wa jina lako; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Amin.

Kasisi: MWENYEZI Mungu, Baba yetu wa mbinguni, ambaye ameahidi msamaha kwa rehema zake nyingi kwao wote wamjiao kwa toba la moyo na imani ya kweli;akurehemuni; akusameheni; akuokoeni na dhambi zenu zote; akutieni nguvu, akuimarisheni katika wema wote; akufikisheni kwenye uzima wa milele; kwa Yesu Kristo Bwana wetu. *Amin*.

Sikieni maneno ya kutia moyo yaliyosemwa na mwokozi wetu Kristo kwa wote wanaomjia kwa kweli.

NJONI kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.
Mathayo 11:28
Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele
Yohana 3:16

Sikieni tena asemayo Paulo Mtakatifu.
Ni neno la kuaminiwa, tena la stahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi.
1 Timotheo 1:15

Sikieni tena asemayo Yohana Mtakatifu.
Kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu
1 Yohana 2:1

Inueni mioyo yenu

Watu: Twaiinua kwa Bwana
Kasisi: Na tumshukuru Bwana Mungu wetu.
Watu: Ni haki, tena ni wajibu wetu

Kasisi: NDIO wajibu wetu, ni haki, tena ni faradhi kwetu, kila wakati na kila mahali, tukushukuru Bwana, Baba Mtakatifu, Mungu Mwenyezi wa milele.
KWA hiyo sisi, pamoja na malaika na malaika wakuu, na jeshi lote pia la mbinguni, twakutukuza na kuliadhimisha jina lako tukufu; tukikusifu daima, tukisema,

Kasisi na Watu: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu wa Majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako. Utukufu una Wewe, Ee Bwana uliye juu. Ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa jina la bwana; Hosana juu mbinguni.
Amin.

Kasisi: MWENYEZI Mungu, Baba yetu wa mbinguni, ambaye kwa wema wako na huruma zako ulimtoa Mwana wako pekee Yesu Kristo afe msalabani kwa ukombozi wetu; ambaye hapo, kwa kujitoa mwenyewe mara moja tu, alitoa dhabihu, na sadaka, na kafara, iliyo timilifu, na kamili, na ya kutosha, kwa dhambi za ulimwengu wote; naye aliamuru, na kutuagiza katika Injiri yake takatifu, tufulize ukumbusho wa daima wa kifo chake cha dhamani, hata atakaporudi; utusikie, Baba wa rehema, twakuomba kwa unyenyekevu, na kwa kuvipokea viumbe hivi vyako, mkate na divai, kwa amri takatifu ya Mwana wako Yesu Kristo Mwokozi wetu, tukikumbuka kufa na kuteswa kwake, utujalie tuushiriki mwili na damu yake vilivyobarikiwa:

Watu: Bwana wetu, uturehemu.

Kasisi: YEYE usiku ule ule aliosalitiwa, alitwaa mkate; na akiisha kushukuru, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akisema; Twaeni, mle, huu ndio mwili wangu utolewao kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.
Vivyo baada ya kula akakitwaa kikombe; akiisha kushukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili yenu na

kwa watu wengi, kwa ondoleo la dhambi: fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. *Amin.*

[Wakati Wakuupokea ushirika Utakatifu]

Kasisi: MWILI wa Bwana wetu Yesu Kristo, uliotelewa kwa ajili yako, ukulinde mwili na roho hata uzima wa milele. Pokea, ule huu, ukikumbuka kuwa Kristo alikufa kwa ajili yako, nawe umle yeye moyoni kwa imani, ukishukuru.

Kasisi: DAMU ya Bwana wetu Yesu Kristo, iliyomwagika kwa ajili yako, ikulinde mwili na roho hata uzima wa milele. Unywe hii ukikumbuka kuwa damu yake Kristo ilimwagika kwa ajili yako, ushukuru.

Watu Wote*:* Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa.
Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amin.

Kasisi: MWENYEZI Mungu wa milele, twakushukuru sana kwa kuwa watukirimia sisi, tulikwisha pokea sisri hizi takatifu, na kutulishachakula cha rohoni, mwili na damu ya Mwana wako, Mwokozi wetu Yesu Kristo, vilivyo vya thamani mno; tena kwamba hivyo umetithibitisha neema yako na wema wako kwetu; tena kwamba tu viungo kweli vya mwili wa siri wa Mwana wako, jamii iliyo heri yao wote waaminio; tena kwamba tu warithi wa ufalme wako wa milele kwa kutukaini, kwa ajili ya kustahili kwa kufa kwenye thamani na kuteswa Mwna wako mpendwa. Nasi twakuomba kwa unyenyekevu, Baba wa mbinguni, utusaidie kwa neema yako ili tudumu katika shirika hili takatifu, tukiyatenda matendo mema yote, uliyotutengenezea tuenende nayo, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Kwake huyo, pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, iwe heshima yote na utukufu wote milele na milele. *Amin.*

Watu: ATUKUZWE Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia. Twakusifu, twakuhimidi, twakuabudu, twakutukuza, twakushukuru, kwa ajili ya utukufu wako mkuu, Bwana Mungu, Mfalme wa mbinguni, Mungu Baba Mwenyezi.
Ee Bwana, Mwana pekee, Yesu Kristo, Bwana Mungu, Mwana kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, uchukuaye dhambi za ulimwengu, uturehemu; uchukuaye dhambi za ulimwengu, ukubali kuomba kwetu; uketiye mkono wa kuume wa Mungu Baba, uturehemu. Maana ndiwe pekee mtakatifu; ndiwe pekee Bwana, ndiwe pekee, Ee Kristo pamoja na Roho Mtakatifu, uliye mwenye adhama katika utukufu wa Mungu Baba. Amin.

***Kasisi*:** AMANI ya Mungu ipitayo fahamu zote; iwalinde mioyo na nia zenu, katika hali ya kumjua na kumpenda Mungu, na Mwana wake Yesu Kristo, Bwana wetu; na Baraka ya Mungu Mwenyezi, Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, iwe kwenu, ikae nanyi daima. *Amin.*